ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 5*** ***10th February, 2023***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 5 Vol. 104 Dated 10th February, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 40 la tarehe 10/2/2023

SHERIA YA TAIFA YA MASHITAKA
(SURA YA.430)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

NOTISI YA UTEUZI WA MWENDESHA MASHITAKA YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itaitwa Notisi ya Uteuzi wa Mwendesha Mashitaka ya mwaka 2023.

Uteuzi wa Waendesha Mashitaka

Sura ya 269

2. Mtu ambaye jina lake limetajwa kwenye Jedwali la Notisi hii ameteuliwa kuwa mwendesha mashitaka kwa madhumuni ya kuendesha mashauri ya jinai kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashitaka kwa masuala yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Usajili wa Wasanifu na Wapima Majengo.

Uhalali wauteuzi

3.-(1) Uteuzi uliofanywa chini ya Notisi hii utakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Notisi hii.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1), mtu aliyeteuliwa kama mwendesha mashtaka anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kinachopungua miaka mitano endapo ajira ya mtu huyo kwenye Utumishi wa Umma itakoma au endapo uteuzi wa mtu huyo utaamuliwa vinginevyo na Mkurugenzi wa Mashtaka.

JEDWALI

UTEUZI WA MWENDESHA MASHITAKA

| NA. | JINA |
|---|---|
| 1. | Ibrahim Mohamed |

Dodoma,
2 Februari, 2023

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU,
*Mkurugenzi wa Mashtaka*